# Kairuki Green IVF yaleta tabasamu, watoto 160 wapatikana kwa upandikizaji D'Salaam

**Na Mwandishi Wetu**

**KITUO** cha kupandikiza mimba cha Kairuki Green IVF (KGIVF), kilichoko Bunju A jijini Dar es Salaam kimefikisha jumla ya watoto 160 tangu kuanzishwa kwake miaka mitatu iliyopita.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa kituo hicho, Dk Clementina Kairuki, wakati akizungumzia maadhimisho ya siku ya kimataifa ya IVF ambayo huadhimishwa kila tarehe 25 Julai kila mwaka.

Alikuwa akizungumza na wasanii wa JUAKALI waliotembelea kituo hicho kujifunza namna kinavyofanya shughuli zake za kupandikiza mimba na kusaidia familia zenye changamoto ya uzazi.

Dk Clementina alisema tarehe 25 Julai imepangwa kuwa siku ya IVF duniani kwani ndiyo siku ambayo mtoto wa kwanza alipatikana kwa njia ya upandikizaji mimba ambaye kwa sasa anamiaka 47.

"Tunawapongeza sana watu waliogundua hii IVF kwasababu haikuwa rahisi kwani waligundua baada ya kujaribu mara nyingi sana, walijaribu karibu mara 103 ndipo wakafanikiwa mtoto wa kwanza akazaliwa, hata magazeti ya wakati ule Uingereza yanaonyesha habari zote ziliandika tukio hilo," alisema

Alisema tangu kuzaliwa kwa mtoto huyo wa kwanza teknolojia ya upandikizaji mimba imekuwa ikiongezeka siku hadi siku na inafanyika kwa njia za kisasa Zaidi kuliko ilivyokuwa ikifanyika miaka ya zamani.

"Mpaka kufikia juzi tarehe 23 Julai tulikuwa na watoto 158 lakini jana wamezaliwa wawili kwenye hospitali ya Kairuki Mikocheni hivyo tumetimiza idadi ya 160 , tunashukuru sana uelewa wa wananchi kuhusu upandikizaji mimba unaendelea kukua siku hadi siku natunatoa elimu," alisema

Alisema watoto waliozaliwa kwa njia ya upandikizaji mwanzoni kabisa baada ya kuanza kituo hicho wameanza shule na wazazi wao wanatoa ushuhuda namna wanavyofanya vizuri wakiwa shuleni.

"Nimefanyakazi kwenye fani hii kwa Zaidi ya miaka 24 kwa hiyo ninauzoefu mkubwa wa kutosha nina furaha kubwa kuona wanawake ambao awali ilishikana kuwapa huduma hii sasa kutokana na teknojia kukua tunaweza kuwapa huduma hii na wakapata watoto," alisema Dk Clementina

Alisema huduma hiyo miaka ya nyuma watu walilazimika kuifuata nje ya nchi kwa gharama kubwa lakini kutokana na kuanzishwa kwa KGIVF watu sasa hawana haja ya kupanda ndege kwenda nje ya nchi kwani huduma hizo watazipata hapa nchini.

"Kituo chetu kimepata ithibati ya kimataifa ya ubora kwasababu kinatoa huduma bora ambazo zingeweza kupatikana kwenye mataifa makubwa yaliyoendelea tena kwa gharama kubwa kwenda kule lakini sasa wakija hapa kwetu wanapata huduma kama hizo,"

# Wajasiriamali wadogo Bagamoyo sasa kicheko, Oryx yawapa mitungi

**Na Mwandishi Wetu**

**KAMPUNI** ya Oryx Gas imekabidhi mitungi ya gesi ya kupikia 600 kwa makundi mbalimbali ya wajasiriamali wakimo mama lishe huku Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo CPA.Subira Mgalu akieleza kuwa uamuzi wa Oryx kugawa mitungi hiyo kunakwenda kuondoa kabisa athari za kiafya zinazotokana na matumizi ya nishati chafu kama kuni na mkaa.

CPA Mgalu ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge na Nishati na Madini ameyasema hayo leo mwishoni mwa wiki katika Tamasha la Samaki wilayani Bagamoyo ambapo kupitia tamasha hilo limetumika kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia pamoja na mafunzo ya matumizi salama ya nishati hiyo.

"Oryx Gas wamekuwa wadau wakubwa katika kuhamasisha nishati safi ya kupikia ya gesi ya LPG kwa vitendo na kupitia Samaki Festival wameamua kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kugawa mitungi ya gesi kwa makundi mbalimbali ya wajasiriamali yakiwemo ya Mama na Baba Lishe.

"Tunafahamu kabla ya Serikali inayoongozwa na Rais Dk.Samia Suluhu Hassan ambaye ni kinara wa nishati Afrika kuja na kampeni ya nishati safi ya kupikia kulikuwa na matumizi makubwa ya kuni na mkaa hali iliyosababisha watumiaji wa nishati hiyo kuwa na athari za kiafya huku watu 32000 wakipoteza maisha kutokana na madhara ya kutumia kuni na mkaa,"amesema Mgalu.

Ameongeza watu walikuwa wanavuna sana miti kwa ajili ya kuni na mkaa na kusisitiza nchi yetu watu wengi wameathirika kutokana na matumizi ya chafu kwa kutumia kuni na mkaa.

"Wameathirika katika mfumo wa hewa , macho yamekuwa mekundu na vufua kuuma lakini Serikali ilikuwa inaingia gharama kutibu walioathirika hivyo Rais Dk.Samia Suluhu Hassan akaja na kampeni ya nishati safi ya kupikia lengo likiwa ni kupunguza au kumaliza kabisa matumizi ya kuni na mkaa nchini.

"Na miongoni mwa nishati safi ni gesi ya majumbani ya LPG na leo Oryx Gas wamekuja kutuunga mkono na kugawa mitungi ya gesi 600 kwa wafanyabiashara ,mama lishe na wajarisilimali wengi.

"Hivyo kama Mbunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kazi yetu Bunge ni kuhakikisha mipango ya Serikali katika Kampeni ya nishati safi inatekeleza."

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Oryx Energies Tanzania Imani Mtafya amesema katika kuunga mkono juhudi za Serikali kuhamasisha nishati safi ya kupikia wamekabidhi mitungi ya gesi 600 yenye thamani ya Sh.milioni 48 kwa makundi mbalimbali ya wajasiriamali.

Pia amesema kuanzia mwaka 2021 hadi mwaka 2026 wameshatoa mitungi 72000 yenye thamani ya Sh.bilioni 5.7 , lengo likiwa kuunga mkono juhudi za Serikali ambayo imeweka lengo ifikapo 2034 watumiaji wa nishati safi ya kupikia wawe wamefikia asilimia 80 kutoka asilimia 29 iliyopo sasa .

Mtafya amesema juhudi wanazofanya zinalenga pia kukomesha utumiaji wa kuni na mkaa ambao unaathiri kubwa sio tu kwa mazingira lakini kwa afya ya mtumiaji huku akifafanua kwasasa wanafanya uwekezaji mkubwa ili kuendana na sera ya Serikali ya kuhamasisha nishati safi ya kupikia.

"Tumewekeza katika ujenzi wa miundombinu ya ghala jipya la kuhifadhi gesi ambalo litagharimu Sh.bilioni 40 ili kuhakikisha tunaongeza usambazaji wetu wa gesi nchi nzima."

Pia amesema katika kuhakikisha kuwa na matumizi salama ya gesi ya LPG ,Oryx Energies wameanzisha idara maalum ambayo itakuwa inatoa elimu ya matumizi salama na sahihi yq nishati safi ya kupikia na elimu hiyo watatoa kwa makundi yote katika jamii pamoja na wanafunzi katika shule na vyuo.

Wakati huo huo Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani Shaibu Ndemanga ameelezea mkakati wao katika kuhamasisha nishati safi ya kupikia na uamuzi wa Oryx Gas kugawa mitungi 600 ni hatua inayoonesha dhamira ya kuachana na kuni na mkaa hasa kwa wakaanga samaki.

# Tanzania yaandika historia nyingine Kimataifa

**Na Benny Mwaipaja, London**

**TANZANIA** imeandika historia mpya katika masoko ya fedha ya kimataifa baada ya hatifungani ya kwanza inayotolewa nje ya nchi (Tanzania off-shore Bond) yenye thamani ya dola za Marekani milioni 100, sawa na takriban shilingi bilioni 262.5 za Tanzania, iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa, mwanachama wa Kundi la Benki ya Dunia (IFC) kwa kutumia sarafu ya Tanzania, kuorodheshwa katika Soko la Hisa la London, Uingereza.

Fedha hizo zimeekezwa Benki ya NMB Plc kwa njia ya mkopo, ambako zitatumika kuwaendeleza kimtaji wafanyabiashara wadogo na wa kati (MSMEs), huku asilimia 20 ya fedha hizo sawa na takriban shilingi bilioni 52.5 zimetengwa kwa ajili ya kuwawezesha wafanyabiashara wadogo wanawake.

Akizungumza kuhusu hatua hiyo, baada ya kupiga kengele kuashiria uzinduzi wa hati fungani hiyo na kufunga biashara ya soko la hisa kwa siku hiyo, Waziri wa Fedha wa Tanzania, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar, alisema mafanikio hayo yanafungua ukurasa mpya wa kuiwezesha Tanzania kujenga imani zaidi kwa wawekezaji wa kimataifa na kupanua vyanzo vya mitaji kwa ajili ya Dira 2050.

"Huu ni mwanzo wa hatua muhimu katika safari ya Tanzania ya kushiriki kikamilifu katika masoko ya mitaji ya kimataifa kwa kutumia sarafu yetu wenyewe. Uorodheshwaji huu unaonesha imani kubwa ya taasisi za kifedha za kimataifa kwa uchumi wetu na mwelekeo wa mageuzi ya sekta ya fedha nchini," alisema Balozi Omar.

Aidha, Mhe. Balozi Omar alisema kuwa uorodheshwaji wa hatifungani hiyo katika soko kubwa na lenye hadhi duniani kama London Stock Exchange, unaipa Tanzania thamani ya kipekee ya sifa na ishara chanya kwa wawekezaji, jambo litakalosaidia kuboresha uwezo wa nchi kukopa na kukopesheka kwa gharama nafuu.

"Lengo letu si tu kuona dhamana hii inafanikiwa katika soko la kimataifa, bali pia kuhakikisha kuwa matokeo yake yanaonekana moja kwa moja katika ukuaji wa sekta binafsi, hususan kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati ambao ni nguzo muhimu ya uchumi wetu," alisema Mhe. Balozi Omar.

Naye Mkurugenzi Mtendaji na Afisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Bi. Ruth Zaipuna, alieleza furaha yake kuhusu hatua hiyo na kwamba fedha zilizopatikana zitasaidia kuchachua uchumi wa nchi kwa kutoa mikopo ya muda mrefu kwa wafanyabiashara wadogo, wa kati, jambo litakaloongeza kasi ya ukuaji wa sekta binafsi, ajira na shughuli za uzalishaji nchini.

"Hii ni mara ya pili kwa benki yetu kunufaika na Soko la Hisa la London ambapo mwaka 2023 tulipata zaidi ya shilingi bilioni 400 kupitia Hati Fungani ya Jamii na sasa tumepata zaidi ya shilingi bilioni 262.5 kupitia hati Fungani ambayo kwa mara ya kwanza imeorodheshwa kwa sarafu ya Tanzania" Alisema Bi. Zaipuna.

Kwa Upande wake, makamu wa Rais wa Benki ya Dunia anayesimamia masuala ya Hazina, Bw. Jorge Familiar, alisema kuwa Benki ya Dunia inajisikia fahari kushirikiana na Tanzania kutimiza malengo yak ya kukuza uchumi wake jumuishi kupitia utekelezaji wa Dira ya taifa ya Maendeleo 2050.

"Tunacho kiangalia sisi si tu kiwango cha fedha tunachowekeza kwa kushrikiana na washirika wetu bali ni matokeo ya uwekezaji huu ambapo tunaamini fedha hizi zitaleta mageuzi makubwa ya kiuchumi na kijamii na tunakadiria kuwa zaidi ya watu elfu 13 hadi 20 wakiwemo wanawake watapata ajira na wakati huo huo wawekezaji wa kimataifa wamepata nafasi ya kuwafikia wafanyabiashara kwa kuwekeza" alisisitiza Bw. Familiar.

Kwa ujumla, uorodheshwaji wa hatifungani hiyo unatajwa kuwa ni hatua ya kimkakati inayoiweka Tanzania katika nafasi bora zaidi ya kushindana katika soko la kimataifa la fedha, huku ukiunga mkono jitihada za kukuza uchumi jumuishi na endelevu.

Benki ya Dunia kupitia Taasisi yake ya IFC, imewekeza nchini Tanzania zaidi ya dola za Marekani bilioni 1.6 ambazo zimekezwa katika miradi mbalimbali ya kimkakati inayokwenda sambamba na malengo ya serikali kuitia seka binafsi katika miradi ya miundombinu, kilimo, masoko ya mitaji na nishati.